JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MALIASILI NA UTALII
WAKALA WA HUDUMA ZA MISITU TANZANIA

MISITU NI MALI

TANGAZO

UUZAJI WA MITI YA MISAJI KWA NJIA YA MNADA KATIKA SHAMBA LA MITI MTIBWA NA LONGUZA

1. Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) unatarajia kuuza miti aina ya Misaji yenye jumla ya meta za ujazo **10,127.174** iliyopo katika shamba ya miti Mtibwa mkoani Morogoro na Longuza mkoani Tanga. Jumla ya meta za ujazo **4,677.637** na **5,449.537** zitauzwa katika shamba la miti Mtibwa na Longuza mtawalia. Miti hiyo iliyopimwa ujazo katika ploti itauzwa kwa mnada kwa kuzingatia kanuni ya 31 (ii) ya Kanuni za Sheria ya Misitu za Mwaka 2004. Miti hiyo ya Misaji itauzwa mahali ilipo na jinsi ilivyo na mnunuzi hatakuwa na haki ya kudai fidia baada ya mauzo.

2. Kampuni au mtu binafsi mwenye nia ya kushiriki mnada anatakiwa kuwasilisha kwenye bahasha iliyofungwa nia yake (rejea sehemu ya 15 ya Tangazo hili) ya kushiriki mauzo kwa njia ya mnada akiambatisha usajili wa kiwanda cha kuchakata magogo au Mkataba na mmiliki wa kiwanda cha kuchakata magogo (2020/2021) kwa asiye na kiwanda hicho, nakala ya cheti cha utambulisho wa mlipa kodi (TIN) na risiti ya malipo (pay-in slip) ya nia ya kushiriki mnada (rejea sehemu ya 13 ya Tangazo hili). Aidha, anatakiwa aoneshe jina la shamba, namba ya kitalu/vitalu na ujazo anaotarajia kununua kama ilivyo kwenye jedwali namba 1 na 2 hapo chini.

3. Mnada utaendeshwa hadharani wakiwepo wanunuzi wote katika ofisi za shamba husika. Mnada katika shamba la miti Mtibwa utafanyika siku ya **Jumatano** tarehe **2 Septemba**, **2020 saa 4:30 asubuh**i na katika shamba la miti Longuza Mnada utafanyika siku ya I**jumaa** tarehe **4 Septemba, 2020 saa 4:30 asubuhi**. Mnada utafanyika kwa kufuata Sheria ya Misitu Sura 323.

4. Kila Kitalu kitanadiwa peke yake kulingana na bei na ujazo uliopo. Hata hivyo, bei ya juu itakayotolewa na mnunuzi mshiriki wakati wa kufungua bahasha ndiyo itakuwa bei ya kuanzia na haitazuia wanunuzi wengine kuongeza bei zao zaidi ya iliyotajwa awali.

5. Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania unawaalika wanunuzi wa miti ya misaji kuwasilisha nyaraka sahihi ili kuwahalalisha kushiriki mnada. Uchanguzi wa viunga vya kuvuna unaweza kufanyika kwa kuzingatia taarifa zilizomo katika jedwali namba 1 na 2 kama ifuatavyo:

JEDWALI Na. 1: ORODHA YA VITALU VILIVYOKO SOKONI VIKIWA NA UJAZO NA BEI - SHAMBA LA MITI MTIBWA

Na.	Jina la kitalu	Ujazo kwa kitalu (M3)	Bei ya kuanzia kwa kila meta ya ujazo (TZS/M3)
1.	LR13 - M	116.956	500,000/=
2.	LR13 - N	120.721	480,000/=
3.	LR13 - O	169.837	550,000/=
4.	LR13 - P	134.316	530,000/=
5.	LR13 - Q	132.270	470,000/=
6.	LR13 - R	380.729	410,000/=
7.	LR13 - S	138.767	410,000/=
8.	LR13 - T	251.707	480,000/=
9.	LR13 - U	304.522	600,000/=
10.	LR13 - V	243.985	480,000/=
11.	LR13 - W	265.208	500,000/=
12.	LR13 - X	181.256	500,000/=
13.	LR13 - Y	416.233	520,000/=
14.	LR13 - Z	464.751	580,000/=
15.	LR13 - A1	197.299	500,000/=
16.	LR 16B - 20	400.310	370,000/=
17.	LR 16B - 23	342.440	310,000/=
18.	LR 16B - 24	129.100	330,000/=
19.	LR16B - 25	147.030	300,000/=
20.	LR16B - 32	140.200	280,000/=
	Jumla	**4,677.637**	

JEDWALI Na. 2: ORODHA YA VITALU VILIVYOKO SOKONI VIKIWA NA UJAZO NA BEI - SHAMBA LA MITI LONGUZA

Na.	Jina la kitalu	Ujazo kwa kitalu (M3)	Bei ya kuanzia kwa kila meta ya ujazo (TZS/M3)
1.	LG9-A1	174.799	650,000/=
2.	LG9-A2	284.787	650,000/=
3.	LG9-A3	192.063	650,000/=
4.	LG9-A4	249.133	650,000/=
5.	LG9-A5	262.583	650,000/=
6.	LG9-A6	315.544	650,000/=
7.	LG9-A7	261.459	650,000/=
8.	LG9-A8	278.035	650,000/=
9.	LG9-A9	277.390	650,000/=
10.	LG9-A10	105.289	650,000/=
11.	LG9-A11	90.477	650,000/=
12.	LG9-A12	306.966	650,000/=
13.	LG9-A13	211.624	650,000/=
14.	LG9-A14	219.420	650,000/=

Na.	Jina la kitalu	Ujazo kwa kitalu (M3)	Bei ya kuanzia kwa kila meta ya ujazo (TZS/M3)
15.	LG9-A15	189.896	650,000/=
16.	LG9-A16	286.103	650,000/=
17.	LG9-A17	152.939	650,000/=
18.	LG8-22	261.850	630,000/=
19.	KH10-10	515.370	720,000/=
20.	KS12- A12	343.090	720,000/=
21.	KS12- A15	299.230	720,000/=
22.	KS12- A24	171.490	720,000/=
	Jumla kuu	**5,449.537**	

6. Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania utatoa barua ya ushindi kwa mnunuzi aliyeshinda kwa kila kiunga.

7. Mnunuzi atakayefanikiwa kununua miti ya misaji hataruhusiwa kusafiirisha magogo nje ya nchi kwa mujibu wa kanuni ya 50 (1) ya kanuni za misitu za mwaka 2004.

8. Wanunuzi wanakaribishwa kutembelea vitalu shambani wakati wa saa za kazi kuanzia saa tatu (3:00) asubuhi hadi saa tisa (9:00) alasiri siku za Jumatatu hadi Ijumaa isipokuwa siku za sikukuu. Meneja wa shamba husika au msaidizi wake atakuwepo kwa ajili ya maelekezo zaidi.

9. Wanunuzi wanapaswa kuchukua na kusoma miongozo ya uvunaji kwa kila shamba. Miongozo hiyo inapatikana ofisi za shamba husika.

10. Bei ya kianzio kwa mita moja ya ujazo imeoneshwa katika Jedwali namba 1 na 2 hapo juu imejumuisha ‘VAT’, ‘CESS’ na ‘LMDA’.

11. Mnunuzi atakayeshinda atatakiwa kulipa asilimia ishirini na tano (25 %) ya thamani yote ya ununuzi ndani ya siku tatu (3) za kazi kuanzia siku ya mnada. Fedha hizo hazitarudishwa. Asilimia sabini na tano (75%) iliyobaki italipwa ndani ya siku kumi na nne (14) baada ya siku ya mnada. Malipo yote yafanyike kupitia Benki au Mitandao ya simu baada ya kupewa hati ya madai (Bill) ya Mfumo wa Makusanyo ya Serikali (GePG) itayotolewa na Meneja wa shamba husika.

12. Mnunuzi atapaswa kuwasilisha hati ya malipo kwa meneja wa shamba husika kama uthibitisho wa malipo siyo zaidi ya siku tatu (3) baada ya malipo kufanyika.

13. Kampuni au mtu binafsi aliyewahi kushinda mnada na kukiuka masharti ya mnada katika minada iliyopita hataruhusiwa kushirikia kwenye mnada

14. Mnunuzi aliyeshinda mnada atatakiwa kuondoa mazao ya misitu aliyonunua ndani ya miezi miwili (siku sitini) baada ya kumaliza kulipa malipo yote kwa asilimia 100.

15. Nia za wanunuzi zilizowekwa kwenye bahasha iliyofungwa ziwasilishwe kabla ya saa 4:00 asubuhi ya siku ya mnada. Aidha, wanunuzi watakaochelewa kuwasilisha nia zao kwa siku na muda uliopangwa hawataruhusiwa kushiriki katika mnada.

16. Tangazo hili pia linapatikana katika tovuti zifuatazo za: www.tfs.go.tz na www.mnrt.go.tz

Limetolewa na
KAMISHNA WA UHIFADHI
S. L. P 40832
DAR ES SALAAM

19.08.2020